# FORM FOUR CLUSTER KCSE MODEL 3

# KISWAHILI PAPER 1 QUESTIONS

1. UFAHAMU: (Alama 15 )

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

1. Miaka ya zamani, kabla ya mabadiliko ya binadamu, ufanisi wa kupata chakula na mahitajimengine ulitegemea ubabe wa mnyama au kiumbe anayehusika. Wale wanyama dhaifu ambaohawana vifua vya kuonyeshana ubabe na wenzao walihasirika pakubwa. Maisha ya aina hii badoyangali miongoni rawa hayawani wanaoishi msituni. Huu hasa ndio msingi wa kauli ya "Kanuni yaporini" hasa pale ambapo sheria haitumiki bali wenye nguvu wanaamua kutumia kifua. Ni nini hasakinachoyadhibiti matendo ya binadamu na kuzima kuwapo kwa kanuni hiyo ya porini?Jibu la swali hilo ni sabali sana: kuwepo kwa katiba ambayo huwa msingi wa kuiongoza jamii. Babualiyependa mchezo wa maneno sana alizoea kutueleza kimzaha, "katiba ipo ili kudhibiti vitiba vyawatu wasije wakawatimba wenzao!" Katiba ni nini lakini?Katiba hutumiwa kueleza mfumo wa serikali ya nchi na hasa kanuni ambazo huunda na kudhibitiutendakazi wa serikali hiyo. Kwa msingi huu basi, katiba inakuwa kama roho ya nchi hiyo; ikiwaitakuwa ambaya basi nao utendakazi wenyewe utakuwa mbaya, kanuni huweza kuwaza sheriaambazo hutambuliwa na mahakama ambazo zina jukumu la kuhakikisha kuwa zimetekelezwa nakufuatwa bila ya ubaguzi wala mapendeleo. Zipo kanuni nyingine ambazo hutokana namaelewano, desturi, itikadi na kaida ambazo hudhibiti jamii inayohusika na huwa sehemu ya hakiza jamii yenyewe.Nchi ambayo inatawaliwa kwa msingi wa katiba hujulikana kama serikali ya kikatiba. Serikaliambayo inatawaliwa kwa kutegemea katiba huheshimu sheria na kanuni zilizopo. Serikali hiyohutumia katiba iliyopo kama msingi wa utendakazi wake na huhakikisha kuwa kila raia wa nchihiyo anaitii na kuiheshimu katiba iliyopo. Kibinimethali cha serikali ya kikatiba ni serikali ya ki-mia.Serikali ya aina hii haiongozwi na sheria zozote bali huongozwa na matakwa na hawaa ya nafsi yakiongozi mmoja au kigaro kidogo cha watu wanaozunguka kiongozi wa aina hiyo. Katika nchi yaaina hiyo sheria zilizopo hutumika kama nyenzo ya kuhalalisha udhalimu na kulilinda tabaka laviongozi na vibaraka wao.Matendo ya serikali ya kikatiba kwa upande mwingine huongozwa na kudhibitiwa na vizuizi fulani.Vizuizi hivi hutokana na kuwako kwa sheria zinazolinda haki ya kila mmoja. Haki hizo hulinda raiawa nchi bila ya kujali rangi, jinsia, maumbile, dini, vionjo wala makazi yake. Jamii ya aina hiyohaiongozwi tena na msemo wa 'mwenye nguvu mpishe' au 'mnyonge kupata ni mwenye nguvukupenda'. Ikiwa mwenye madaraka atakiuka sheria zilizopo, ataadhibiwa bila ya mapendeleo.Mnyonge naye akikiuka sheria ataadhibiwa vivyo hivyo.Hapo kabla

tulilinganisha katiba ya nchi na roho ya nchi hiyo. Nchi ambayo haina roho ni nchiiliyokufa na isiyotegemewa kuwa na uhai wowote. Hii ina maana kuwa, katiba kutegemewa kunamambo kadha ya kuzingatia. Msingi wa katiba nzuri ni ufahamu wa raia kuwa nchi yao ina hadhikubwa kuliko wao wenyewe. Katiba nzuri ni ile ambayo itakuwa na uwezo wa kuilinda jamii hiyokwa kipindi kirefu. Haihalisi kuwa na katiba ambayo itatumika miaka michache kisha baadayeisiweze kufaa tena. Vivyo hivyo ni haramu mutlaki kwa katiba kuwepo kwa muda ili kuyakidhimahitaji ya kundi fulani la watu ambalo litakuwepo kwa muda tu. Ni misingi ipi basi muhimu katikakuunda katiba ya aushi?Msingi wa kwanza na wa lazima ni uzalendo, uzalendo unakuwa nguzo kuu kwa kuwa,tunapozungumzia katiba ya nchi fulani humaanisha inahusu jamii fulani inayojitambua kama yataifa fulani. Uzalendo ni hisia ya kuipenda nchi yako kwa dhati na kuwa tayari hata kuifia. Ikiwahisia za uzalendo ni dhati, basi itakuwa rahisi kwa jamii inayohusika kuiwazia katiba ambayoitaendelea kuwako kwa miaka mingi ijayo. Jamii inayoongozwa na hisi za uzalendo na utaifahaitakubali kupofushwa na tamaa za muda tu. Msingi mwingine muhimu ni utambuzi wa kuwajamii inawajulisha watu wa kila aina na wenye tofauti anuwai. Tofauti hizi zinaweza kuwa zakirangi, kilugha, kiidadi, kielimu, kijinsia, kimaumbile, kiuwezo n.k. Katiba nzuri lazima itiliemaanani uhalisi huo na iuakisi.Katiba haina budi kutambua kuwa jamii ina historia yake na hasa utamaduni na upekee wake.Kuna baadhi ya matendo ambayo ingawa yamezoeleka kwingine ni mageni na yanatisha katikautamaduni mwingine. Kwa mfano uhusiano wa kimapenzi kati ya mwanamume na mwanamumemwenzake (yaani ubasha) na kati ya mwanamke na mwanamke mwenzake (usagaji), hamna nchiambayo inashabihiana na nyingine katika ngazi zote. Uhalisi huu lazima uwepo katika katiba yanchi inayohusika. Haimakiniki kufuata sheria na kanuni za nchi ajinabi au mataifa mengine kwakuwa yameendelea tu. Hii haina maana kuwa jamii haiwezi kukopa mambo fulani yanayowezakuifaidi. La hasha, inaweza. Lakini kukopa nako kunahitaji kuchuja yapi yanafaa na yapi yanaihasirijamii. Ni muhimu kujua kuwa kiini cha katiba yoyote ile ni uwezo wa jamii wa kujiamulia mamboyao ya kuyaendesha ipasavyo. Lau sivyo, tutawapa wengine nafasi ya kutumia vitimba vyao kututimba si si.

a) Toa kichwa kinachoafiki taarifa hii. (alama 1)

......................................................................................................................................................
.............

b) Eleza maana ya katiba kwa mujibu wa taarifa hii. (alama 2)

.................................................................................................................................... .................
......................................................................................................................................................
.............

c) Eleza vigezo VINNE vinavyopaswa kuzingatiwa wakati wa kuunda katiba ili idumu muda mrefu.(alama 4)

……………………………………………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………………………… ……………
…………………………………………………………………………………………………………………………
………….

d) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika taarifa. (alama 3)

i. Hawaa na nafsi. ……………………………………………………………………………………………

ii. Kibini methali ……………………………………………………………………………………………

iii. Katiba ya aushi ……………………………………………………………………………………………………

f) Nchi isiyokuwa na katiba nzuri inaweza kukumbwa na matatizo yapi? (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………… ……………
…………………………………………………………………………………………………………………………
……………………

2. UFUPISHO: (Alama 15 )

Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali.

Vijana ni kundi linalounda asilimia kubwa ya idadi ya watu nchini Kenya. Hii inamaanisha kuwamaamuzi yote yanayofanywa nchini lazima yazingatie maoni ya kundi hili muhimu. Lakini swali nije, maoni ya vijana yamezingatiwa? Vijana wa nchi hii wamekumbwa na shida chungu nzima kwasababu sera ya serikali kuhusu vijana ni hafifu sana.Katika nchi ya Kenya, tumeona serikali ikijaribu kufanya juhudi kuwasaidia vijanahivyo basiMgalla muue na haki umpe. Mfano mwafaka ni kuwa serikali iliunda Wizara ya Vijana na hapobaadaye ikabuni Hazina ya Maendeleo kwa Vijana (NYDF). Hazina hii ilipewa jukumu la kuhakikishavikundi vya vijana vimeundwa ili kupata ufadhili kutoka kwa serikali kwa minajili ya kuanzishamiradi ya kujikimu kimaisha na kuongeza ajira kwa vijana. Katika hatua ya mwanzo, serikali ilitoashilingi bilioni moja kwa hazina hii ili kutolewa kwa makundi ya vijana kupitia mashirika mbalimbaliya kifedha. Jambo hili lilifanyika lakini swali ni je, pesa hizi ziliwafikia watu waliokusudiwa?Pia Wizara ya Vijana ilipanuliwa na kuongezewa Idara ya Michezo, kwa sababu michezohuwahusisha vijana wengi sana. Hivyo basi usimamizi mzuri wa michezo utaamua iwapo vijanawatapata afueni katika changamoto zinazowakabili katika maisha. Ombi la vijana kwa waziri mpyakatika Wizara ya Vijana na Michezo ni kupiga msasa usimamizi wa michezo ili kuwafaidi vijanaambao ni wengi sana humu nchini.Usimamizi mzuri wa sekta zote zinazowahusisha vijana utasaidia kuwazindua vijana na kuwapamatumaini katika maisha. Pia serikali inafaa kuwapa kipaumbele vijana katika ajirkatika Utumishiwa Umma au katika Mashirika ya Serikali. Dhana kuwa VIJANA NDIO VIONGOZI WA KESHO inafaakutupiliwa mbali na mahala pake kuchukuliwa na dhana kuwa VIJANA NDIO VIONGOZI WA JANA,LEO NA MILELE. Ni ajabu sana kwa sababu kuna watu waliokuwa uongozini nilipokuwa na umri wamiaka mitatu, wakasema kuwa mimi ni kiongozi wa kesho, na bado hawajang'atuka. Swali ni je,kesho haifiki?Hatima ya vijana itaamuliwa na jinsi serikali itakavyobuni sera kuwahusu vijana hawa. Sera nzuri

zitaondoa utamaushi miongoni mwa vijana katika maisha. Kutamauka huku huwafanya vijanakujihusisha na vitendo kama uraibu wa vileo, ukahaba,ujangili,ubakaji miongoni mwa vitendovingine vya kihalifu.

Mipango ya kuwainua vijana katika maisha inafaa kufanywa kwa ushirikiano kati ya Wizara ya Fedha, Wizara ya Vijana na Michezo na washikadau wengine husika. Ni kupitia juhudi hizi ambapo vijana watasaidika na kuacha kushiriki katika vitendo vya uvunjaji wa sheria. Juhudi hizi zote zitafaulu tu ikiwa serikali itakuwa na ile ari ya kuwaauni vijana ambao ni asilimia 70 ya idadi yawatu humu nchini.

a) Fupisha aya kwanza tatu kwa maneno 30 – 40. (alama 4 + 1 mtiririko)

Matayarisho

.................................................................................................................................. ................

.................................................................................................................................. ................

.................................................................................................................................. ................

..........................................................................................................................................................

.................................................................................................................................. ................

.................................................................................................................................. ................

.............

Nakala safi

............................................................................................................................................. ......

.................................................................................................................................. ................

..........................

b) Vijana wanakumbwa na changamoto zipi nchini Kenya kulingana na kifungu hiki? (Maneno40-50) (alama 5+1 mtiririko)Matayarisho

Nakala safi

c) Ni mikakati gani serikali inafaa kuchukua ili kusaidia vijana? (Maneno 20-30) (alama 3 + 1mtiririko) Matayarisho

...........................................................................................................................

Nakala safi

.................................................................................................................... ............................

.................................................................................................................... ............................

.....................................................................................................................................................

.................................................................................................................... ............................

……………………………………………………………………………………………………… ……………………….

3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40 )

3. a) Weka maneno yafuatayo kwenye ngeli zake: (alama 1)

i. Gulio

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

ii. Ghubari (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

b) Tunga fungu tenzi kamilifu na uonyeshe viambishi awali vya;

i. Urejeshi (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

ii. Ukanushi (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

c) Tunga sentensi mbili kutofautisha vitate vifuatavyo.

i. Shamba (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

ii. Chamba (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………….

d) Kwa kila kihishi kilichotajwa, tunga sentensi kubainisha matumizi yake.

i. Thubutu! (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………….

ii. Aaa! (alama 1)

……………………………….

e) Fuata maagizo uliyopewa

i. Geuza neon lililo pigwa mstari katika sentensi kuwa kielezi

Kasi yake ya uandishi inatisha. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………….

ii. Geuza neon lililopigwa mstari kuwa kiwakilishi.

Mtoto mbaya aliadhibiwa. (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………….

f) Tumia vitenzi hivi kutunga sentensi kulingana na kauli uliyopewa

i. Unga (kutendama) (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………….

ii. Wa (kutendewa) (alama 1)

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………….

g) Onyesha shamirisho kipozi na shamirisho kitondo katika sentensi ifuatayo. (alama 2)

Kampuni ile imewalipa wafanyakazi wake mishahara mizuri

………………………………………………………………………………………………………………………………

……………………………………………………………………………………………………………………….

h) Kanusha sentensi hizi

i. Kuliko na vita ni kule kulichochewa na wanasiasa. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………….

ii. Kanusha sentensi hii kwa kuzingatia sehemu iliyopigiwa mstari.

Utakapokuwa mkubwa utayaelewa mambo haya. (alama 1)

……………………………………………………………………………………………………………………….

.....................................

i) Taja sauti mbili zinazotamkwa kwa ushirika wa ulimi na ufizi. (alama 2)

……………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………….

j) Bainisha mofimu katika neon lifuatalo (alama 2)

k) Kwa kutoa mifano eleza matumizi manne ya herufi za mlazo. (alama 4) ………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………..

……………………………………………………………………………………………………………………….

……………………………………………………………………………………………………………………….

JUMA: Mama!Ulinipata wapi mimi?

MAMA: Nilikuzaa, juma.

Andika upya katika usemi wa taarifa ambapo mama Juma anamweleza Baba Juma juu ya mazungumzo haya. (alama 4)

……………………………………………………………………………………………………………………….

.....................................

……………………………………………………………………………………………………………………….

…………………………………………………………………………………………………………………………

m) Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi zifuatazo.

i. Vijana kwa wazee walikusanyika ukumbini. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

ii. Kakake alifanya kazi hiyo kwa ufasaha. (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

n) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya mistari. (alama 4)

Mwalimu mrefu mweusi alipigwa jana na wakora.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

o) Vifungie sentensi viunganishi hivi

i. Seuze (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………………

ii. Mingairi ya (alama 1)

…………………………………………………………………………………………………………………………

p) Geuza sentensi ifuatayo kwa udogo kasha iandike katika wingi (alama 2)

Mtoto amelala ndai ya nyumba kwa sababu anaogopa nyoka

q) Tunga methali mojai kutokana na taarifa ifuatayo. (alama 2)

Mtoto akidekezwa sana tabia yake itakuwa mbaya ikiwa mtu mzima.

…………………………………………………………………………………………………………………………

…………………………………

…………………………………………………………………………………………………………………………

.....................................

4. ISIMU JAMII: (Alama 10 )

Huku ukitoa mifano mwafaka, eleza maana ya istilahi zifuatazo kama zinavyotumika

katika isimu Jamii.

a) Lingua franca (alama 2)

.........................................................................................................................................................

...............................................

b) Rejista (alama 2)

....................................................................................................................... ............................

....................................................................................................................... ............................

...............................................

c) Pijini (alama 2)

....................................................................................................................... ............................

.........................................................................................................................................................

d) Krioli (alama 2)

....................................................................................................................... ..

e) Diglosia (alama 2)

........................................................................................................................ ............................

.........................................................................................................................